

Ufaafu wa Jalanda Tamthilia kigogo

- Anwani kigogo ina maana – mtu mwenye madaraka makubwa ya kiutawala
- Anwani yenyewe imeandikwa kwa herufi ndogo ,kashiria kuwa kiongozi aliyshikilia mamlaka hatadumu milele.
- Pia imeandikwa kwa rangi ya majano kuashiria kuwa hata ikiwa uongozi wa kigogo majoka ni wa kukandamiza ,bado pana tumaini la ustawi.
- Jalanda lenyewe ni la rangi ya kijani pande zote mbili.Hili linaashiria kuwa eneo la sagamoyco lina ustawi mkubwa ambalo umekaliwa na kigogo majoka aliye mamlakani.
- Katika sehemu ya chini kila ,pana picha ya mtu aliye kalia kiti,amevalia kofia kichwani ,kashika tama kwa mkono mmoja na kashikilia rungu kwa mkono mwingine

Hili ni taswira ya kigogo Majoka.

- Juu pana picha ya kikundi cha watu waliokongamana .Hili linaashiria wana Sagamoyo wanaodamana ili kufunguliwa soko la chapakazi wanaongozwa na Tunu na Sudi.
 - Pana mwangamaza juu ya wale watu walioandamana kuashiria kuwa ,harakati zao za kupigania Uhuru wa Sagamoyo zinafua dafu.
 - Maelezo yaliyoandikwa katika sehemu ya nyuma ya Jalanda yameandikwa kwa rangi ya majano kuashiria kuwa pana tumaini kubwa la watu wa eneo la sagamoyo
- Ukirejelea jalanda la tamthilia kigogo jadili maudhui katika tamthilia kigogo

Dhamira ya mwandishi wa Tamthilia Kigogo

- Pauline kea ambaye ndiye mwandishi wa tamthilia kigogo anadhamiria kuonyesha hadhari za uongozi mbaya hasa kwenye mfumo mpya uliozinduliwa nchini Kenya mfumo wa ugatuzi.
- Pia anadhamiria kuonyesha harakati za wapiganiaji haki za kibinadamu na matatizo wanayoyapitia katika harakati zao.
- Pia anaonyesha shida wanazozipata wananchi maskini,wasio na uwezo wa kujitetea
- Mhusika mkuu Majoka Bin Marara ambaye ndiye kigogo wa Sagamoyo anatumiwa kuwakilisha viongozi dhalimu wanaotumia mamlaka yao vibaya na kukandamiza haki za wananchi wa kawaida.
- Wanahusika Tunu na Sudi wametumiwa kuwakilisha wanaharakati wanaopigania haki za binadamu kwa udi na uvumba.

MAUDHUI

Mwandishi Pauline Kea ameangazia maudhui mbalimbali katika tamthilia yake kigogo. Dhahadhi ya maudhui haya ni pamoja na:

- ✓ Uongozi mbaya na hathari zake.
- ✓ Ulevi
- ✓ Elimu
- ✓ Umaskini
- ✓ Mapinduzi
- ✓ Utabaka
- ✓ Nafasi ya mwanmke
- ✓ Mapenz
- ✓ Kazi
- ✓ Ndoa na familia
- ✓ Utu
- ✓ Ukatili
- ✓ Usaliti

- ✓ Ufisadi
- ✓ Utamaduni

Maudhui ya uongozi mbaya

Haya ndiyo maudhui makuu katika tamthilia ya Pauline Kea.

Mwandashi ameangazia maudhui haya kwa mawanda na mapana sana.

Amemtumia mhusika mkuu Majoka bin Marara kama kielelezo cha kiongozi dhalima wasio karibu nao.

Mhusika Majoka anatumia nafasi yake kuanzisha kampuni nyingi za kibinafsi kama vile *Majoka and Majoka company na Majoka and Majoka Resort*.

Anatumia mamlaka yake kuarisha vyombo vya dala kumtumikia .Anamwamrisha Kingi ambaye ni mkuu wa polisi pale Sagamoyo kumpa walizi wa kutosha na kuwatumia askari kupigana na waandamanaji pindi wanapopanga maandamano dhidi yake.

Pia anatumia vikaragozi kama vile ;Mzee Kenya ,Chopii ,Ngurumo ,Boza ,Mamapima,(Asiya) n.k kuendeleza utawala wake dhalimu.

Mfano:Anamtumia mzee Kenya kupata ushauri kwa jinsi ya kutekeleza maovu.

Pia anamtumia kumshawishi Sudi kumchongea kinyango ambayo ni njia mojawapo ya kuthiihirisha Ubinafsi wake.

Anawatumia Ngurumo na Asiya kueneza uvumi kwa wananchi katika lile deni ya unywaji pombe pale Mangweni.Hii ilikuwa ni njia mojawapo ya kutuliza mioyo ya wanachi waliofungiwa soko la chapakazi.

Maudhui ya Uongozi mbaya

- Uongozi mbaya wa Bwana Majoka ulileta athari mbaya katika jimbo la Sagamoyo.
- Kwanza kabisa soko la chapakazi ambalo lilikuwa kitega uchumi kikuu cha wanasagamoyo lilifungwa na kuleta umaskini si haba.
- Matumizi ya uongozi na mamlaka vibaya yalileta wemavu kwa Tunu aliyevamiwa na genge la Bwana Majoka aliyewaongoza walevi wengine kuwaumbua Tunu na Sudi.
- Ulevi unaathiri jamii ya Sagamoyo vibaya kwa kuwa hawapigi hatua mbele kimaendeleo.

Maudhui ya ulevi

- Asiya ambaye pia anajulikana kama Mama Pima alitengeneza pombe haramu pale Mangweni na watu wengi waliishia kwenda kupiga mtindi pale kwa soko la chapakazi tayari lilikuwa limefungwa.
- Ngurumo ambaye alikuwa shabiki mkuu wa Bwana Majoka aliwaongoza walevi wengine kuwaumbua Tunu na sudi.
- Ulevi unaathiri Jamii ya Sagamoyo vibaya kwa kuwa hawapigi hatua mbele kimaendeleo.

Maudhui ya kazi

- Mwandishi Pauline Kea ameyashughulikia maudhui ya kazi kwa magwanda mapana katika tamthilia yake kigogo.
- Sudi komb na Boza ,ni wachongaji vinyago kazi ambayo wanaifanya ili kukimu familia zake.Wanafanya kazi hii kwa bidii na weledi mkuu.
- Ashua bibiye Sudi alifanya kazi ya kuchuuza mandazi ,chai na maembe pale sokoni chapakazi na hata baada ya soko kufugwa alizurura huku na kule kuuza bidthaa zake ndipo aweze kukimu mahitaji ya familia yake.
- Wafanyakazi wengine ambao wameangaziwa katika tamthilia ya kigogo ni pamoja na:*Dactari na Nesi* ambao wanafanya kila juhudi kuyaokoa maisha ya Bwana Majoka.
- Kingi ambaye ni mkuu wa polisi pia anatekeleza wajibu wake kwa njia inayofaa ili kuyalinda maslahi ya wananchi katika jimbo la Sagamoyo.
- Chopi ambaye alikuwa mlinzi na tarishi wa Bwana Majoka alitekeleza wajibu wake kwa njia inayofaa na kwa bidii mno.Ndiye alimfahamisha Bwana Majoka kuhusu mauko ya mwanawe Ngao Junior.

Maudhui ya Elimu

- Mwandishi Pauline Kea ,ameyashughulikia maudhui ya elimu kwa mawanda mapana katika tamthilia yake kigogo.
- Wahusika Sudi ,Tunu na Ashua wamesoma na kuhitimu mpaka chuo kikuu .Wanatumia elimu yao kama kigogo kikuu cha kulete mabadiliko katika jimbo la Sagamoyo ingawa wote wamesoma na kuhitimu ,hakuna aliyeajiriwa rasmi. Jambo ambalo linaonyesha uozo wa uongozi mbaya wa Bwana Majoka.
- Ngurumo ambaye ni shabiki mkuu wa majoka alishindwa na elimu katika darasa la kwanza.Pia alimchukia sana mwalimu wa historia lakini anaishia kuwa mojawapo wa washauri wakuu wa Majoka jambo ambalo ni kinaya kikuu cha maisha.

Umaskini

Mwandishi Pauline Kea ,katika tamthilia yake kigogo ameyaangazia maudhui ya umaskini kwa mawanda mapana .Hata kama Sudi na Ashua wamesoma na kuhitimu mpaka chuo kikuu ,hawana ajira nzuri na wanashindwa kutimiza mahitaji yao ya kimsingi kama vile kuwalea wana. Baada ya kufunguliwa kwa soko la chapakazi ,wengi wa wananchi wa Sogamayo wanaishi katika umaskini mkubwa.Umaskini huu unawafanya kwenda kupiga mtindi kwa mama pima(Asiya)

Uongozi mbaya wa Bw.Majoka ndiyo chanzo cha umaskini uliokithiri katika lile sehemu la Sagamoyo.

Maudhui ya utabaka

Mwandishi Pauline Kea ameshughulikia maudhui ya utabaka kwa mawanda mapana katika tamthilia yake kigogo.

Kuna matabaka mawili makuu yanayojitokeza .Tabaka la walalaheri na walalahoi.

B.w Majoka ,Kenya ,Kingi na pia Tunu wamo katika tabaka la walalaheri .Wana mali ya kutosha yanayoweza kukithi mahitaji yao ya kila siku na kubakisha ilhali wanasagamoyo kama vile Boza ,Kombe Sudi ,Arusha ,Asiya ,Ngurumo ,Siti wamo katika tabaka la walalahoi. Ni vigumu kwao kukithi mahitaji yao ya kila siku na inawabidi kuchapa kazi kwa bidii ila wanaisha kula makombo .Maneno ya Susi: *''Mimi sili makombo kama Keibu. ''nishakunywa chai ya mke wangu nikarithika(uk 13)*

Utabaka uliopo katika jimbo la Sagamoyo unapatishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine B.w Majoka amemilika uongozi na utajiri wake kutoka kwa babake B.w Marara .

Pia anataka kupitisha ukwasi ule kwa mwanawe Ngao Junior ambaye anaishi kuliwa .`kukuoza Ngao Junior akitoka kutoka ngambo wiki chache zijazo ,wakuonaje?maneno ya B.w Majoka (uk 41).`Usitazame kwa moyo Tunu .Tazama kwa macho uione kesho .Ione fanaka kwa Ngao .`Maneno ya Majoka .(uk 42)

Maudhui ya mapenzi na ndoa

- Mwandishi Pauline Kea ,katika tamthilia yake ameyashughulikia maudhui ya mapenzi na ndoa kwa mapana na marefu.
- Kuna mapenzi ya dhati baina ya Ashua na Sudi .Ashua alizitupilia mbali sinikizo za B.w Majoka ambaye ni mkwasi na kumfuata Sudi amabaye ni Kabwela .Hilo ni dhibitisho la mapenzi ya dhati .Ingawa wanachangamoto nyingi ndoa inastahimili na kufua dafu.
- Ndoa ya Majoka na Husda haijanjengwa kwa misingi ya fedha na samani .Kuna mtafaruku mkubwa katika ndoa ile.Majoka anaeleza kuwa ,Husda hakumwoa kwa sababu ya mapenzi mbali alimwoa kwa ajili ya mali..`Nyanya tafadhali Husda hanipenda ,anazipenda mali zangu .Hayo si mapendo ya dhati .`Maneno ya Majoka (uk 75).Ndoa hii inadoa kwa kuwa Majoka anampenda Ashua bibiye Sudi jambo ambalo linaleta mtafaruku mkubwa sana.`leo nitaua mtu

mie ,nitakumaliza Ashua.”Majoka haonekani kwake kasa na maana ni wewe.Huwezi kunitoa tonge kinywani hivi hivi.Umenizidi nini kwani?”Maneno ya Husda kwa Ashua.(uk 26)

- Ndoa ya Boza na Asiya .Ndoa baina ya Bozaa na Asiya inamashaka mengi.Je! Asiya ni mke mwenye wake ,Boza au Ngurumo?Je! katika ndoa hii nani mwenye sauti ,Boza au Asiya?“*Asiya ni wangu .Wako au wa Ngurumo?*”(uk 64) Maneno ya Sidi.“*Wetu sisi sote ,pili pili usioila yakuashia ni?*Maneno ya Ngurumo.
- Usuba baina ya Tunu na Sudi .Urafiki uliokuweco baina ya Tunu na Sudi una maswali mengi sana .Je! hawa wawili ni wapenzi?Je! Sudi anampenda Ashua au Tunu?

Nafasi ya mwanamke katika Jamii

- Mwandishi Pauline Kea ameyashughulikia maudhui ya nafasi ya mwanamke katika jamii kwa mawanda mapana sana.Amechora mwanamke kwa pembe zote mbili. Kwanza amemchora kama chombo cha mapenzi kinachotumiwa kukithi kiu cha mwanaume .Pia amecmchora kama chombo cha kuleta mapinduzi na mabadiliko katika jamiii
- Mwanamke kama chombo cha mapenzi .Majoka anajaib kumtumia Ashua kama chombo cha mapenzi .“*Mimi sili watu ,sitakuuma .Siwezi nikakudhuru .Kitu aali cha tunu kama wewe .Nikulinganashe na nini?Urembo wako hauna mfanowe Ashua.*” (uk.20)
- Ngurumo anamtumia Asiya kama chombo cha mapenzi..“*Kwamba Asiya aliupata mradi wa keki kwa kukupa uroda ?*” (uk.64)“*Ndio maanake wanaziita keki za uroda ?*”
- Husda pia anatumiwa na mumewe kama chombo cha mapenzi.“Majoka and Majoka modern resort yapata saa tatu asubui.Majoka ameketi kwenye ubao wa kukalia amevaa fulana na kaptura.Anakunywa sharubati ya mchungwa .Mkewe Husda anajiunga naye kwenye ubao akiwa na mavazi ya kuogelea ambayo yameloa maji .Amefunga kitambaa maridadi kichwani.Anachukua miwani nyeusi kutoka kwenye kibweta chake kasha anakaa kando ya Majoka (uk.67).
- Mwanake kama chombo cha mapinduzi na mabadiliko .Mwandishi Pauline Kea anawatumia wahusika Tunu ,Ashua Siti na Hashima kama kielelezo cha mabadiliko katika jamii.
- Tunu alipigana kwa ulimi na mate kumwangusha Kigogo Majoka.
- Ashua ,Siti na Hasima pia wanachangia pakubwa katika uongozi dhalimu Majoka.
- Mchango wao ni muhimu sana,katika jamii yeyote ile .Jambo ambalo linaonyesha juhudi wanazozipitia wanawake katika ukombozi wao.

Maudhui ya ulemavu

Mwandishi ameyashughulikia maudhui ya ulemavu katika tamthilia yake kigogo.

Mhusika Tunu anaishia kuwa mlemavu baada ya kuvunjwa uti wa mgongo na genge la Bw Majoka lililoongozwa na Ngurumo.Hashima na Siti wanamwinua Tunu na kumweka kwenye kiti cha magurudumu.(uk 53)

Maudhui ya utu

- Pauline Kea ameyaangazia maudhui ya utu katika tamthilia yake kigogo.
- Mhusika wa kiepiki babu ametumika kuhusitu ukatili wa Majoka na kuonyesha umuhimu wa utu.Tunu na Sudi wanaongozwa na utu kuzipigania haki za wanasagamoyo.
- Wahusika wengine wenye utu ni Siti na Hashima wanaomsaidia Tunu katika hali yake ulemavu.
- Daktari na Nesi wanamuudumia Bwana Majoka kwa utu mwingi sana.
- Inspekta wa polisi Kingi pia ni mhusika mwenye utu.Anakataa kuyafuata maagizo ya Bw.Majoka ya kuwaangamiza wana Sagamoyo.Anatambua umuhimu wa haki zao na anafahamu kuwa sharia za inchi zinawalinda.
- Ashua pia ni mtu mwenye utu .Anawapelekea chakula Boza,Sudi na kombe.Pia anahisi uchungu wa wanawe pendo na pili wanapokosa chakula.

Maudhui ya ukatili

- Mwandishi Pauline Kea ameangazia maudhui ya ukatili katika tamthilia yake kigogo kwa mapana na marefu.
- Mhusika B.w Majoka ana ukatili mwingi sana. Anapanga jama za kuwakandamiza wanamapinduzi kama vile Sudi, Tunu, Ashua na Siti.
- Ngurumo pia ni katili. Anakiongoza kikundi kilichotumwa na Majoka kumlemaza Tunu.
- Kenga pia ni katili. Wanashirikiana na BW. Majoka kupanga jama za vifo vya watu kama Ngurumo.
- Kufungwa kwa soko pia ni ukatili mkuu kwa kuwa ulikatiza riziki za wanasagamoyo wengi.

Maudhui ya ukaragozi

Pauline Kea ameyashughulikia maudhui ya ukaragozi katika tamthilia yake kigogo.

Wahusika kama vile Kenga, Ngurumo, Chopi, Boza na Asiya wote ni vikaragozi wa Bw. Majoka. Wanatumiwa kuendeleza uongozi dhalimu.

Maudhui ya ufasadi

Mwandishi Pauline Kea ameyashughulikia maudhui ya ufasadi katika tamthilia yake kigogo.

- Mhusika mkuu Bw. Majoka anatumia nafasi yake kunyakua mali ya umma na kujinufaisha (kujitayarisha). Anawapokonya wanasagamoyo sosko la chapakazi na kudhamiria kujenga hoteli ya kifahari pale. Pia anajitajirisha kwa kampuni yake itwaje Moajoka and Majoka company, Majoka and Majoka resort na Majoka and Majoka Academy.
- Anawatmbilea marafiki zake wa karibu na kwapa ``keki`` Bw. Kenga anatumiwa kupelekea Sudi ``keki`` ndiposa achonge kinyango Bw. Majoka.

WAHUSIKA NA SIFA ZAO

A. MAJOKA

- ✓ Ni kiongozi wa jimbo la Sagamoyo.
- ✓ Ni mumewe Husda.
- ✓ Ni babake Ngao Junior.
- ✓ Ni mwanawe Bw.Marara.
- ✓ Ni mjukuu wake Ngao.
- ✓ Ni mmiliki wa Majoka and Majoka company,Majoka and Majoka resort na Majoka Academy.

SIFA ZAKE

I. Ni katili

Anapanga jama ya kumlemaza Tunu.Pia anawaagiza askari kuwatawanya waandamaji wanaotetea sosko la Chapa kazi.

Pia anawatuma ``chatu’’ kumwangamiza Ngurumo.

II. Ni fisadi

Anamtuma Bw.Kenga na ``keki’’ kwa Sudi ,Boza na Kombe ,ndiposa wamchongee vinyango.

III. Ni mware

Ingawa ana bibi Husda ,anamtamani sana Ashwa bibiye Sudi na kujaribu kumshawishi ampe uroda.

IV. Ni mpyoro

Anapenda kutumia maneno ya matusi sana.``*shut up ! woman wasaliti nyinyi hamna shukrani hata mpigieni huyo Tunu wenu kura tuone hata msiponipa kura moja nitashinda.*’’ (uk.91).

“*Utakaa hapa name ,sitaki hawa makunguru wanidhuru.*”(uk 38)

V. Ni Jasiri

Anaujasiri wa kujitokeza kaika umati wa watu hata kama amewakosea na wamekasirika naye.

VI. Ni mwizi

Anatumia cheo chake kunyakua mali ya umma.Anafunga soko la chapakazi kwa lengo la kujenga hoteli la kifahari.

VII. Ni mbinafsi

Anatia maslahi yake mbele ya matakwa ya wanasagamoyo waliomchagua.

VIII. Ni mwenye majuto

Baada ya kuzirai aliposikia kifo cha mwanawe Ngao Junior ,katika ule uigizaji wa kiepiki anajuta matendo ya nafsi yake na kumwomba babu yake ushauri.

IX. Ni msiri

Anahifadhi siri nyingi ambazo hataki kuzielekeza moja kwa moja kama vile uhusiano wake na Ashua ,unyakuzi wa mali ya umma kuendeleza kampuni ya Majoka and Majoka company n.k

Umuhimu wake

- a. Ni kielelezo cha viongozi wasiowajibika katika uongozi wao haswa barani Africa .Viongozi wanaotumia mamlaka yao kujitayarisha na kulidhi mahitaji yao ya kibinafsi.
- b. Ametumiwa kuukashifu mfumo wa ugatuzi unaoongozwa na viongozi wenye tama ya fisi.

B. TUNU

- ✓ Ni mwanamapinduzi
- ✓ Ni mwanawe Hashima
- ✓ Ni rafiki yake Sudi ,Ashua na Siti.

SIFA ZAKE

I. Ni mwenye utu

Anaongozwa na utu kuzipigania haki za kimsingi za wanaSagamoyo

II. Ni msomi

Amesoma na kuhitimu chuo kikuu kule Nga'mbo.Ili linatokea katika kejeli ya wimbo wake Daudi Kabaka aliouimba Ngurumo.

“Msichana mrembo kama wewe ni kitu gani kinachofanya usiolewe ,elimu unayo ya kutosha hata Ng'ambo ulieda ukarudi.”(uk 65)

III. Ni jasiri .

Anapambana na Majoka kwa ujasiri na kukashifu matendo yake hata baada ya kulemazwa na genge alilolituma Majoko lililoongozwa na Ngurumo.

IV. Ni mwenye mapenzi ya dhati.

Anawajali watoto wake Sudi (Pendo na Pili) na kumwagiza Siti awapeleke kwa mamake ili awatunze .(uk 18)

V. Ni mwana mapinduzi

Anashiriki katika harakati za kuikomboa Sagamoyo kutoka mikononi mwa Kigogo Majoka.

VI. Ni mrembo

Urembo wake unajidhihirisha kutokana na kejeli yake Ngurumo kutoka kwa wimbo wake Daudi Kabaka.

Umuhimu wake

- a. Ni kielelezo cha vijana waliosoma wanaoshiriki katika harakati za mapinduzi na kuzikomboa nchi zao kutoka mikononi mwa vigogo dhalimu.
- b. Ni kielelezo cha wananchi jasiri wanaojitolea kufa kupona kwa ajili ya haki z kibinadamu .
- c. Yey kulemazwa ni dhihirisho la watu ambao wako tayari kupatwa na lolote kwa minajili ya ukombozi wa nchi zao.

C. SUDI

- ✓ Ni mchonga vinyago.
- ✓ Ni mumewe Ashua.
- ✓ Ni babake Penda na Pili
- ✓ Ni rafikiye Tunu na Siti.

SIFA ZAKE

I. Ni msomi

Amesoma na kuhitimu chuo kikuu.

II. Mwenye bidii.

Anafanya kazi ya kuchonga vinyago ndiposa awezi kukimu mahitaji ya familia yake.

III. Ni mwenye mapenzi ya dhati.

Anampenda bibiye Ashua kwa moyo na mapenzi ya dhati.

Anaenda kumtembelea anapofungwa na Majoka.

IV. Ni jasiri

Anapigania haki za wanaSagamoyo bila woga wowote na kuwakabili Majoka na vikaragozi wake moja kwa moja ,kwa ushujaa mwingi .”Mimi sili makombwe kama kelbu ,nishakunywa chai ya mke wangu nikariridhika.”(uk 13)

V. Ni mwenye utu

Anajali maslahi ya wanasagomoyo waliofungiwa soko la chapakazi ndiposa anashiriki katika harakati za kutetea ufunguzi wa soko lile.

VI. Ni mkweli

Anamsimamo dhabiti na anawatambua mashujaa halisi wa Sagamoyo .”Nawe muugwana wamchonga nani?” “Shujaa halisi wa Sagamoyo.” (uk 10)

VII. Ni mwanamapinduzi

Anashiriki katika harakati za kumnyanyua kigogo Majoka.

Umuhimu wake.

- a. Ni kielelezo cha watu wenye bidii maishani wanaofanya kazi kukimu mahitaji ya familia zao.
- b. Oia ni kielelezo cha wasomi wanashiriki katika harakati za ukombozi wanachi zao kutoka mikononi mwa vigogo.

D. ASHUA

- ✓ Ni bibiye Sudi.
- ✓ Ni mamake Pendo na Pili.
- ✓ Ni rafikiye Siti na Tunu.

SIFA ZAKE

I. Ni mwenye bidii

Anafanya kazi kwa bidii ndipo aweze kukidhi mahitaji ya familia yake.”Ndio hali ya maisha bibiye tena lazima tutie tonge kinywani na tuwape wananchi wenye nchi kitu kidogo .Biashahara iko vipi kwenye vioski vyenu?”(u.k 2)

II. Ni mlezi mwema.

Anafanya kila juhudi ndipo aweze kuwalea wanawe Pendo na Pili tendo linalompeleka ofisini mwa Majoka.

III. Ni mwenye utu

Anamsimamo dhabiti na kukataa rai zote za Majoka ikiwemo ile ahadi ya kupewa kazi katika shule ya Majoka and Majoka Academy .”Siwezi ,siwez kufanya kazi kweny kampuni ya kihuni kama hiyo mimi.” (uk 25)

IV. Ni msomi

Amesoma na kuhitimu chuo kikuu.”Na hiyo ndio shida hasa ! Takwimu zako wazitoa visivyo .Ulipofuzu nilikupa kazi katika Majoka Academy ukakataa.Shahada yako ya ualimu ukataka iozee huko sokoni .Sasa ungekuwa mwalimu mkuu katika mojawapo ya shule zetu za kifahari.Maisha yako yangkuwa tofauti kabisa .Utayakaanga marimgo yawe kitoweo wewe siku moja ! (u.k 25)

V. Ni mwanamapinduzi

Anashirikiana na mumewe Sudi ,Tunu na Siti katika harakati za kuikomboa Sagamayo kutoka mikononi mwa kigogo Mojoka .Katika ule mkutano pale sokoni anaongoza katika wimbo wa mapinduzi(uk.92) “Soko lafunguliwa bila nyoka ×2

Soko lafunguliwa bila chopi ×2

VI. Ni mrembo

Ana urembo ambao unamvutia sana bwana Majoka na kumtia hamu ya uroda.

Umuhimu wake

- a. Ni kielelezo cha wanawake wanaopitia changamoto kuu katika ndoa zao sababu ya kupingana na uongozi dhalimu.
- b. Pia ni kielelezo cha wasomi wanaokosa kazi kwa sababu ya kushikilia msimamo dhabiti.

E. SITI

- ✓ Ni dadake Kombe.
- ✓ Ni rafikiye Tunu ,Sudi na Ashua.

Sifa zake

I. Ni rafiki wa dhati

Anashirikiana na Tunu katika hali zake zote hata anapokuwa mlemavu Siti yuko pale kumsaidia

II. Ni mwanamapinduzi

Anashirikiana na Tunu ,Sudi na Ashua kumnyanyua kigogo Majoka.

III. Ni mwenye msimamo dhabiti

Anapoiacha pombe na angali nyuma hata baada ya kushawishiwa na Ngurumo kushiriki katika unywaji wa pombe .”Nawaelewa msitafune maneno sote tulianza kama nyinyi .Safari ni hatua kwa hatua (kwa Siti)Do ! Sitiiii.....nilijua utarudi ,umekumbuka zabibu....”sikuja kunywa pomb mie ,niliacha.....(uk 57)

Umuhimu wake

- a. Ni kielelezo cha marafiki wa dhati walio simama na watu katika hali zote kufa kupona.

F. BOZA

- ✓ Ni mumewe Asiya
- ✓ Ni kikaragozi cha Majoka
- ✓ Ni mchonga vinyago.

SIFA ZAKE

- I. Ni kikaragozi
Anamtumikia na kumpigia upato Bwana Majoka ambaye ni kiongozi dhalimu.
- II. Ni mwenye bidii
Anafanya kazi ya kuchonga vinyago.
- III. Ni mlevi
Anashiriki pombe inayopikwa na bibiye Asiy (Mama Pima)
- IV. Ni mkengeuzi
Anamruka kombe na kumnyima haki yake waliyopewa na Bw Kenga. ``Salamu zako tulizipokea mzee na tuko katika.....``maneno ya Boza.
``Salamu gani?``Maneno ya Kombe.(uk 9)

Umuhimu wake

- a. Ni kiwakilishi cha watu wanaowatumikia na kuwanyenyekea viongozi bila kutazama ukweli uliopo.

G. KOMBE

- ✓ Ni kakake Siti.
- ✓ Ni mchanga vinyago.

SIFA ZAKE

- I. Ni mwenye bidii
Anafanya kazi ya kuchonga vinyago
- II. Ni kikaragozi
Anampigia madebe kigogo Majoka.
- III. Ni mwenye kushawishika haraka
Anashawishika na Sudi na kubadili msimamo wake kumhusu Majoka.

Umuhimu wake.

- a. Ni kielezo cha watu wa kawaida katika jamii wanaopotozwa na uongozi mbaya lakini baadaye wanazidiwa baada ya kupata ukweli wa mambo.

H. NGURUMO

- ✓ Ni kikaragozi cha Majoka.

SIFA ZAKE

- I. Ni kikaragozi
Anamtumikia na kumpigia debe kigogo Majoka.
- II. Ni mkware.
Anashirika urada na mama Pima ambaye ni bibiye Boza. ``Wako au wa Ngurumo.`` Maneno ya Sudi
``wetu sote pili pili usioila yakuashia ni?`` (uk 64)
- III. Ni mlevi
Anashiriki ulevi wa pombe kwa mama Pima na ndiye anayewaongoza walevi wengine.
- IV. Ni katili
Anawaongoza vijana wengine kumvamia Tunu kwa maagizo ya Bw Majoka. ``Mimi nina shughuli zangu Tunu ,hayo aliyoyasema tulishayajua na hayajatushtua.Tafadhali nenda kama hutaki.....Hakuna asiyejua .(Akiashiria miguu ya Tunu)Nilifikiri hila ni funzo tosha.``maneno ya Ngurumo (uk 63)

Umuhimu wake

- a. Ni kiwakilishi cha vijana ambao wanatumiwa na viongozi kuendeleza uongozi dhalimu.
- b. Ni kielezo cha vijana ambao hawashiriki katika shughuli za kujnga taifa hila wanashiriki ulevi.

I. KENGA

- ✓ Ni msichana mkuu wa Majoka.

SIFA ZAKE

I. Ni kikaragozi

Anamtumikia kigogo Majoka bila kuwajali wanasagamoyo.

II. Ni katili

Anashiriki katika kupanga jama ya kumlemaza Tunu.

III. Ni binafsi

Anayajali maslahi yake mwnyewe ndio maanake anamshauri Majoka bila kujali hisia za wahasagamoyo wa kawaida .Lengo lake kuu ni kushibisha tumbo lake na kupata sehemu kubwa ya “keki.”

IV. Ni mshauri mbaya

Anampa Bw Majoka ushauri mbaya wa kupotosha.

V. Ni mkengeuzi

Mambo yanapoharibika anamgeuka Majoka na kuwaunga mkono wanasagamoyo wa kawaida.

VI. Ni mwenye busara

Ana busara nyingi ingawa anaitumia vibaya kumshawishi Sudi kumtumikia Majoka.

UMUHIMU WAKE

- a. Ni kielezi cha watu wanaotoa ushauri mbaya kwa viongozi na mambo yakienda mrama wanawageuka.

J. MAMA PIMA (ASIYA)

- ✓ Ni bibiye Boza.

- ✓ Ni mgema .

SIFA ZAKE

I. Ni kikaragozi

Anamtumikia na kumoigia debe kigogo Majoka.

II. Ni mkware

Anapata sabuni ya kupika keki kwa kuishiriki uroda na Ngurumo.

III. Ni mlevi

Anashiriki katika ulevi pale Mangweni.

IV. Ni gwiji wa kejeli

Anatunga nyimbo nyingi za kuwakejeli Tunu na Sidi.

V. Ni mgema

Anashiriki katika harakati za kutengeneza pombe haramu amabayo inawadhuru wanajamii.

VI. Ni mwenye majuto

Anaishia kujuta matendo yake aliyoyatenda .“*Wamenimaliza wamenigeuka .Pombe yote wameimwanga !Nilijua ninawaponza nilijua ninawapunja nilijua ninawadhuru wanasogomoyo lakini nilimezwa na tama .Najuta zaidi ya kujuta .Naomba msamaha ,Tuna ,naomba radhi wanasogomoyo.Naomba ulinzi wenu .Wananiwinda ,”maneno ya mamapima(uk.92)*

UMUHIMU WAKE

- a. Ni kielezo cha wanajamii ambao hawajali maslahi ya wengine na wanafanya chochote kupata pesa bila kujali wengine .Hana utu.

K. HUSDA

- ✓ Ni bibiye Majoka

- ✓ Ni mamake Ngao Junior

SIFA ZAKE

I. Ni mkali

Anamkasirikia Ashua anapomfumania ofisini mwa Bwanake Majoka.

II. Ni mrembo

Anapenda kujipondoa na kuvaa mavazi ya kuvutia

III. Ni mwenye jicho la nje

Anamtamani chopi wakiwa pale Majoka and Majoka resort (Husda anarejea .Anapomwona chopi anatembea kwa madaha .Amevaa nguo zilizombana na viatu vyenye vichuchumio virefu.Uso wake umejaa vipodozi .Angali ana miwani myeusi .Anamtazama Chopi kwa macho ya uchu kasha anakaa kando ya Majoka) (uk 70)

IV. Ni mwenye tama

Anaingia katika ndoa na Bwana Majoka ,si kwa sababu anampenda ila ni kwa sababu ya mali. *“Nyanya tafadhali Husda hanipendi ,anapenda mali zangu .Hayo sio mapendo ya dhati .”*Maneno ya Majoka (uk 75).

UMUHIMU WAKE

- a. Ni kielelezo cha wanawake wanaoingia katika ndoa kwa sababu ya mali bali si upendo.
- b. Pia anawakilisha baadhi ya wanawake wa viongozi na changamoto wanazozipitia katika ndoa zao.

L. CHOPI.

✓ Ni tarishi na mlinzi wa Majoka.

SIFA ZAKE

I. Ni kikaraguzi

Anamtumikia Majoka na kummundumia bila kuuliza swali lolote.

II. Ni msiri

Anaziifadhi siri za Majoka.

III. Ni mwenye bidii

Anafaya kazi yake ya utarishi kwa bidii mno.

IV. Ni mvumilivu

Anavumilia upyoro na ukali wa Bwana Majoka anapomuundumia

V. Ni mpyoro

Anamzungumzia Sudi vibaya anapompeleka kumwona Ashua jela alikofungiwa na Bw Majoka.

“Toka nisikutoe ,shamba likikushida kulima sema.”(uk 50)

“Hamjamaliza kupigana Kisi?”Muda wenu umekwisha nian kazi ya kufanya.” (uk 50)

UMUHIMU WAKE

- a. Ni kielelezo cha watu wanawatumikia viongozi bila kuuliza maswali.
- b. Pia ni kielelezo cha walinzi katili

M. HASHIMA

✓ Ni mamake Tunu

SIFA ZAKE

I. Ni mwenye mapenzi ya dhati.

Anapenda mwanawe Tunu kwa dhati na kumshughulikia sana katika hali yake ya ulemavu.

II. Ni jasiri

Amevumila mateso mengi kutoka kifo cha bwanake hadi kulemazwa kwa mwanawe Tunu.

III. Ni mwenye bidii

Amevuna mchele mwingi jambo linaloashiria bidii yake shambani.

IV. Mwenye utu.

Alikubali kuwatunza Pili na Pendo walipotumwa kwake na Tunu.

UMUHIMU WAKE

- a. Ni kielelezo cha kina mama wenye utu na wenye mapenzi ya dhati kwa wanao.

- b. Pia ni kielelezo cha kina mama wanaojua uchungu wa kupoteza waume wao kwa sababu ya uongozi mbaya.

N. KINGI

- ✓ Ni mkuu wa polisi.

SIFA ZAKE

I. **Ni mwenye bidii**

Anafanya kazi yake kwa bidii mno.

II. **Ni mkakamavu**

Anakataa kufuata amri za Majoka na kuwafuata wananchi

Anamkabili Bw Majoka moja kwa moja bila woga hata anapatishiwa kuachishwa kazi.

III. **Ni mwenye utu.**

Anajali haki za msingi za wanachi na kuwalinda wakati wanapoandamana.

UMUHIMU WAKE

- a. Ni kielelezo cha polisi wachache weny utu na wanaolinda haki za kimsingi za wananchi.

O. BABU

- ✓ Ni mhusika kiepiki

- ✓ Ni babu yake B.w Majoka.

SIFA ZAKE

I. **Ni mhusika kiepiki**

Anatokea ndotoni.

II. **Ni mkweli.**

Anaisuta nafsi ya Majoka kwa kumweleza mambo kinagubaga.

III. **Ni mwenye utu.**

Anajaribu kumzidua na kumuonyesha Majoka umuhimu wa kuwa na utu.

IV. **Ni mwenye busara**

Anatumia maneno yaliyojawa busara kuisuta nafsi ya Majoka.

UMUHIMU WAKE

- a. Ametumiwa kudhihirisha utamaduni wa kiafrica unaoshikilia kuwa kuna uhai baada ya kifo na kuwa matendo yetu huwaadhiri waliokufu

- b. Ametumiwa kusuta uongozi mbaya unaondelezwa na viongozi wengi duniani.

P. DAKTARI

- ✓ Ni daktari wa Majoka.

SIFA ZAKE

I. **Ni mwenye bidii**

Anatekeleza wajibu wake wa daktari kwa bidii mno na kumuhudumia Bw Majoka kwa njia inayofaa.

II. **Ni mwenye busara**

Anapogundua kuwa Majoka anazungumza na babu yake anaiga ile nafasi ya babu moja kwa moja.

III. **Ni mwenye utu.**

Anajaribu kumtuliza Majoka na kupima maneno yake asiye akamuumiza Husda mke wake .

UMUHIMU WAKE.

- a. Ni kielelezo cha wafanyikazi wanaowajibika katika kutimiza jukumu lao.

Q. NESI.

- ✓ Ni muuguzi wa Majoka.

UMUHIMU WAKE.

- a. Ametumiwa kumjenga daktari na kudhihirisha umuhimu.

R. MTU 1 NA MTU 11

I. Ni mlvi

Wanalewa pale Magweni pa Mama Pima.

UMUHIMU WAO.

1. Wametumiwa kumjenga mhusika Ngurumo na kumkejeli Sudi na Tunu

S. PILI NA PENDO

- ✓ Ni watoto wa Ashua na Sudi.
- ✓ Wametumia kudhihirisha changamoto wanazozipitia Sudi na Ashua.

T. MWANGO

- ✓ Ni askari katika makazi ya Majoka.

SIFA ZAKE

I. Ni kikaragozi

Anamtumikia Majoka bila kuuliza maswali.

UMUHIMU WAKE.

- I. Ni kielelezo cha askari wanaowatumikia viongozi wabaya na kuendeleza uongozi wao dhalimu.

U. MJUMBE

- ✓ Ni mtangazaji katika sauti ya mashujaa.
- ✓ Ametumiwa kuendeleza uongozi dhalimu na ukoloni mamboleo.

MBINU ZA LUGHA NA MBINU ZA SANAA

Mbinu za sanaa.

- ✓ Hizi ni mbinu amabazo hudhihirika moja kwa moja na huifanya kazi ya mwandishi kuvutia.
- ✓ Mbinu kuu aliyoitumia Pauline Kea katika tamthilia yake kigogo n i:-

1) Nyimbo

Twajivunia Saga ni jimbo letu tukufu

Jimbo tunalolipenda daima.....

Sagamoyo tunalilinda ,daima.....

Twamtukuza Ngao kiongozi wetu shupavu

Kwake Ngao tunasujudu ,daima.....

Ngao wetu twakuhusudu ,daima.....(u.k 5)

Msichana mrembo kama wewe

Ni kitu gani kinakufanya usiolewe ?

Elimu unayo ya kutosha hata ng'ambo

Ulienda ukarudi

Ukionyesha majivuno kwa vijana,

Utazeeka ukiwa nyumbani kwenu,

Oooh bebi ,miaka yaenda mbio sana

Nayo sura yako inachujuka,

Pengine tabia zako ndizo mbaya awali

Kweli dada ulijivuna (uk 65)

Sosko lafunguliwa bila nyoka ×2

Soko lafunguliwa bila chopi ×2 (uk 92)

Mbinu za lugha.

- ✓ Mbinu za lugha hujulikana kama tamathali za usemi.huwa na maana fiche.
- ✓ Na iana mbili msomaji usoma kwa makini ndiposa awwe kuzitambau.
- ✓ Baadhi ya mbinu za lugha alizozitumia mwandishi Pauline Kea katika tamthilia ya kigogo ni pamoja na :

- Majazi
- Kinaya
- Kejeli
- Visengerembele
- Visengerenyuma
- Methali
- Semi
- Misemo
- Tashbihi
- Jazada
- Takriri n.k

Majazi

Anwani kigogo ni anwani ya kimajazi .Inawakilisha kiongozi aliye na mamlaka Fulani na jinsi anavyotumia hayo mamlaka kuwakandamiza wananchi wa kawaida.

Majoka

Jina Majoka ni la kimajazi

Nyoka ni mnyama mwenye sumu anayeuma na kuua

Mhusika Majoka katika tamthilia ya Kigogo ana tabia nyingi za nyoka.

Anatimia mamlaka yake kuwakandamiza na kuwaua watu kwa mfano :

- Alihusika katika kifo cha jabali aliyekuwa kiongozi katika chama cha mwenge na mpinzani wake mkuu.
- Pia alihusika katika kifo cha ngurumo.
- Pia alipanga njama ya kumlaza Tunu.

Tunu

- Tunu pia ni jina la kimajazi.
- Tunu kwa kawaida ni zawadi.
- Mhusika Tunu ni zawadi kwa wakazi wa Sagamoyo.
- Ndiy anayewakomboa kutoka mikononi mwa kiongozi dhalimu Majoka.
- Anafanya kila juhudi na mwishowe kuwaletia wanasagamoyo kiongozi.

Sagamoyo

- Sagamoyo pia ni jina la kimajazi.
- Kusaga ni kufanya kitu kama nafaka kiwe unga au vipande vipande kwa kutuia kifaa Fulani kama vile jiwe au mashine .Ni kuponda au kutwanga.
- Moyo ni mtima
- Uongozi mbaya wa kigogo Majoka umesaga mioyo ya wakazi wengi wa eneo la sagamoyo.

Chapakazi

- soko la chapakazi pia ni jina la kimajazi.
- Wanasagamoyo wengi kama vile Ashua walichapakazi katika lile soko na kupata riziki yao ya kila siku.

Sudi

- Sudi pia ni jina la kimajazi maana halisi ya Sudi ni bahati njema.
- Mhusika Sudi katika tamthilia ya kigogo alikuwa bahati njema kwa wakazi wa Sagamoyo kwa kuwa alipigania haki zao.

Boza

- Boza ni jina la kimajazi.
- Maana halisi ya jina Boza ni mtu mpumbavu.
- Mhusika Boza alikuwa mpumbavu sana na alifuata sela za Majoka bila kufikiria.

Ngurumo

- Hili pia ni jina la kimajazi.
- Kuguruma ni hali ya kutoa sauti ya kutisha na yenye kusababisha maafa.
- Mhusika Ngurumo amesababisha maafa mengi katika eneo la Sagamoyo.
- Ikiwemo kulemazwa kwa Tunu.

Husda.

- Husda ni mtazamo wa ubaya juu mtu na mali yake.
- Ni tabia ya mtu kutopendeza na kutofuraha mafanikio ya mwingine.
- Jicho mbaya.
- Husda hakupendezwa na mafanikio ya mumewe na ungo lake kuu ilikuwa ni kupata yale ya mumewe.

LAKABU

Mhusika Asiye amepewa jina la kupangu au lakabu mamapima

Methali

Mwandishi Pauline Kea ameshughulikia mbinu hii ya lugha sana katika tamthilia yake kigogo.

Baadhi ya methali alizotumia ni :

1. *Kuwa asiyjua maana haambiwi maana (uk. 3)*
2. *Ukitaka kula asali kaa na nyuki (uk.7)*
3. *Maskini akipata matako hulia mbwata (uk.7)*
4. *Achanikaye kwa mpini afi njaa .(uk.9)*
5. *Jitihada huvuta heri (uk.9)*
6. *Chelewachelewa utampata mwana si wako .(uk.9)*
7. *Dawa ya deni ni kulipa .(uk 11)*
8. *Usiegeze kwenye inda utavuna hila .(uk 11)*
9. *Mavi ya kale hayaachi kunuka.(uk .12)*
10. *Usijitome kwenye bahari mchafukonge usioimudu mbizi yake (uk.12)*
11. *Mla ni mla leo mla kesho kalani ? (uk.14)*
12. *Aketiye na cha upele haishi kujikuna .(uk .15)*
13. *Kuvuja kwa pakacha ni nafuu kwa mchukuzi .(uk 21)*
14. *Samba hageuki paka kwa kukatwa na kucha. (uk 21)*
15. *Kipanga ndiye hakimwa kwa kesi ya kuku (uk 26)*
16. *Dalili ya mvua ni mawingu (uk 34)*

Mbinu ya kuchanganya ndimi.

Mwandishi Pauline Kea ametumia mbinu hii kwa mawanda mapana katika tamthilia yak kigogo.

- ❖ *Hatutembei na mashine za eskrei .Urembo ni wa nje period .(uk 10)*
- ❖ *Boza stop it .(uk .11)*
- ❖ *Kaa hapo , I know am in bad books but.....twendeni (uk.15)*
- ❖ *Nilikuwa ndani ninakofanyia kazi Majoka and Majoka wamewaua .(uk 160)*
- ❖ *Jukumu la kulinda uhai ,kulinda haki ,kulinda uhuru .Look at the bigger picture man!Hujasahau mafanikio ya mapambano yetu kama viongozi wa chama cha wanafunzi chuoni .(uk.18)*
- ❖ *Uliyoyavulia nguo sharti uyaoge .Kesho ya pili na Pendo na watoto wengine iko mikononi mwetu .its for their good ! (uk.18)*
- ❖ *Na hiyo ndio shida hasa .Takwemu zako wazitia na kuzitoa visivyo .Ulipofuzu nilikupa kazi katika Majoka and Majoka Academy ukakataa .(uk 25)*
- ❖ *Nitahushughulikia muimo wao kwanza .Tunu na Sudi ni wawili but one stone is enough! (uk.36)*
- ❖ *Hata hawana haya.Live coverage ? (uk.38)*
- ❖ *Yes Sir ! Hata risasi.(uk 38)*
- ❖ *Kuta zako zina maskio maskio .Najua unanirekodi haidhuru.Majoka and Majoka company si yako..(uk43)*
- ❖ *Baby damu.....wamekufanyaje honey ? chopi chopi chopi atanitambua.(uk 47)*
- ❖ *Ashuu ,pole sweetie.Kama kosa ni langu .Wajua nakupenda .Kwa nini waliku....(uk.47)*
- ❖ *Uliacha mtindi ukabobea katika drama ? Acha kutoonyesha video hapa .Mashangingi twawajua.(uk 58)*

Maswali Balagha

Mwandishi Pauline Kea amtumia mbinu hii kwa magwanda mapara katika tamthilia yake kigogo.

Baadhi ya mifano ni :

- *Sasa embe la mwenzio linanuka kuliko haya ?uoni wameligeuza soko letu uwanja la kmwagia chemkali na taka ? (uk. 2)*
- *Hicho kijiredio kwenye kijirununu cha pesa nane nacho kinakutia kiburi ? (uk 7)*
- *Unalidharau gogo lililokurusha mto ,sio ? (uk 7)*
- *Kazi ya kuchonga watu wasiojulikana usuli nayo ni kazi ?(uk 8)*
- *Kesho ni ya Mungu ,mla ni mla leo mla kesho kalani ? (uk 14)*
- *Wanatingi Siti ,si soko lilifungwa juzi ?(uk 16)*
- *Hatauzia wapi vinyago na soko limefungwa ?(uk.18)*
- *Niangelie ,niambie ni nini nisichonacho katika milki yangu isipokuwa wewe tu ? (uk.20)*
- *Hivyo vichekechea vyenu viwili vimewashinda ?(uk.22)*
- *Warukaye kama kiroboto ?Hivyo ndivyo unavyosema na umpedaye!(uk 28)*
- *Eti mapenzi ! Aliyekudanganya yanapikiwa watoto ubwabwa ni nani? (uk.24)*
- *Yaani kusema kwamba mapenzi hayatiwi nyunguni na kutokozwa kama mahindi na maharagwe ni tusi tena ?(uk 24)*
- *Unaifukia kesho yetu .Unatupoka utu na heshima .Huoni hivyo Majoka ?(uk 25)*

Tashbihi

Mwandishi Pauline Kea ameiangazia mbinu hii ya lugha kwa mapana na marefu katika tamthilia yake kigogo.

- ✓ *Huku kugaragara kwako kama kuku anyetaka kutaga (uk.1)*
- ✓ *Wewe nawe wapenda kubaki nyuma kama mkia wa kondoo.(uk.5)*
- ✓ *Una mke na bado unafuatana kama mtu na kivuli chake.(uk.6)*

- ✓ *Warukarukaje kama kiroboto (uk 23)*
- ✓ *Jamani ,mimi ni wa kulinganishwa na Samsoni myahudi ama shujaa iyongo wa waswahili (uk 24)*
- ✓ *Tuacheni kufumbatia maji kama jiwe (uk 63)*
- ✓ *Sina muda wa kufikiria mambo ya watu walio akhera ,nafikiria maneno matamu kama asali (uk 70)*
- ✓ *Siku hizi wake hawashikiki ni kama masikio ya sungura!(uk 77)*
- ✓ *Kuishi kulivyo ni kama mshumaa (uk 83)*
- ✓ *Ni lazima kama ibada kuisoma bahari na kusonga mbele kwa mpango kwa kuwa hatuna budi kuishi .(uk 84)*
- ✓ *Kwa tama mtu amepnda kula kuku huku nduguze wakila kama kuku .(uk 84)*
- ✓ *Huwezi kuandamana na wavuvi kama kitoweo hukitaki ! (uk.57)*

Kuhamisha ndimi

Ni mbinu ya kuchukua kauli ya lugha nyingine moja kwa moja na kuitia makala ya lugha tofauti. Mwandishi Pauline Kea ameshughulikia mbinu hii ya lugha katika tamthilia yake ya kigogo.

- ✓ *“yes Sir” maneno ya mwango (uk 29)*
- ✓ *“what “ maneno ya Majoka (uk 35)*
- ✓ *“over my dead body “ maneno ya Tunu(uk.45)*
- ✓ *“shut up woman “maneno ya Mojoka kwa Husda (uk 27)*

Misemao na semi

Mwandishi Pauline Kea ameshughulikia hizi mbinu mfano:

- *Shika yako kombe husijaze susu kwa yao kuhusu .(uk .1)*
- *Kuwa moshi utazaa moto .(uk 3)*
- *Huchuguze pia alacho nyuki husijitie najisi .(uk 7)*
- *Husihesabu vifaranga wako kabla ya kuaguliwa*
- *Sudi ,mbio za Tuna ni za sakafuni (uk.12)*
- *Nilijia tu ! uo hujasiri wenu wa Peni tisa (uk 12)*
- *Maskini jeuri (uk 13)*
- *Udongo haubishani na mfinyazi (uk.13)*
- *Sasa wataka kufanya kichunguu kionekane mlima! .(uk 14)*
- *Shika hamsini zako wewe Sudi (uk 14)maneno ya Boza.*
- *Umekuwa wali wa daku la mno?(uk 19)maneno ya Mojoka kwa Ashua.*
- *Humerudi eh!Ashua aa ,kuonja asali kutoka kuchonga mzinga?(uk 21)maneno ya Majoka kwa Ashua.*
- *Siku zote binadamu humuani kuku na kumhiri kunguru ,wajua kwa nini ?(uk.22)maneno ya Majoka kwa Ashua.*
- *Leo nitaua mtu mie ,nitakumaliza Ashua :Majoka haonekani kwake kisa na maana ni wewe .Huwezi kunitoa tonge kinywani hivi hivi.Kwani umenizidi nini kwani ?(uk 26-27)*
- *Nani asiyemjua mkeo huyu mdaku ? Msambazaji wa kanda za umbea kwenye vikao vya masengenyo(kwa Husda)tuliza nyayo kwako (uk 28)*
- *Nataka kujua mbivu na mbichi za Ashua kuja hapa kwanza (uk 28)*
- *Amesoma sharia lakini nafikiri ni mganga wa siasa(uk 32)*
- *Dalili ya mvua ni mawingu lazima tuwe macho.(uk34)*

MASWALI

1. Jadili ufaafu wa jalada la tamthilia kigogo (ala 20)
2. Mabadiliko ni kama mawimbi baharini hayazuiliki. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia kigogo (ala 20)
3. Ugatuzi ni unyakuzi .Jadili kauli hii ukirjelea tamthilia kigogo (ala 20)
4. Jadili umuhimu wa wahusika wafuatao (ala 15)
 - a. Ashua
 - b. Ngurumo
 - c. Asiya.
5. Usitukane mkunga na uzazi ungalipo .Una bahati sana nakupenda
 - a. Eleza muktadha wa dondoo hii (ala 4)
 - b. Tambulisha tamathali ya usemi katika dondoo hii (ala)
 - c. Eleza sifa nne za msemaji (ala 80
 - d. Eleza changamoto alizopitia msemewa na wenzake katika harakati za mapinduzi (ala 6)
6. Fafanua matumizi ya tamathali za usemi zifuatazo.
 - a. Methali (ala 4)
 - b. Tashbihi (ala 4)
 - c. Jazanda (ala 4)
 - d. Misemo (ala 4)